USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI



# SERA YA KUIMARISHA UWEZO WA WAZAWA



Jifunze zaidi kupitia
https://www.usaid.gov/local-capacity-strengthening-policy

Picha (Iliyo Hapo Juu) kwa Hisani ya: Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa(USAID)/Nepal (Manju)
Picha ya Jalada kwa Hisani ya: Aicha Zarrouk; Afisa Mawasiliano wa MIPA, USAID/Moroko

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| Muhtasari wa Utendaji | 2 |
| I. Maono ya Pamoja ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa | 4 |
| II. Kanuni za Mipango Yenye Ufanisi ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa | 7 |
| III. Kanuni za Ubia Wenye Usawa katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa | 15 |
| IV. Kufanya Mabadiliko Kuwa Kaida ya Taasisi: Mwelekeo wa Kusonga Mbele | 22 |

# MUHTASARI WA UTENDAJI

Maendeleo endelevu yanategemea wadau kutoka katika sekta mbalimbali kuongoza juhudi za kuboresha jamii zao na kufanya kazi kwa umoja na pamoja ili kutimiza malengo ya juhudi hizo. Kwa sababu hii, Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kimekuwa kipengele cha msingi cha mipango ya USAID. Uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa unaweza kupelekea ukuaji wa kiuchumi wa pamoja; maendeleo ya mapema ya huduma muhimu za afya, chakula na lishe, na huduma na mifumo ya elimu; na kukuza utawala wa kidemokrasia. Kuimarisha Uwezo wa Wazawa pia kunaweza kushughulikia sababu zilizopo za udhaifu, kuimarisha mifumo ya ndani ya kuhudumia matukio ya kibinadamu, na kuongeza ustahimilivu dhidi ya mishtuko na mifadhaiko. Kutokana na hilo, uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa husaidia nchi kuzuia, kupunguza na kupata ahueni baada ya migogoro. Hatimaye, uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali ni kigezo muhimu cha mafanikio ya USAID na washirika wake katika kufikia na kudumisha mafanikio ya kibinadamu na maendeleo duniani kote.

### UFAFANUZI MUHIMU

**Uwezo** unajumuisha maarifa, ujuzi, na motisha pamoja na mahusiano yanayomwezesha mhusika—mtu, shirika au mtandao—kuchukua hatua ili kubuni na kutekeleza suluhisho kwa changamoto za ndani za maendeleo, kujifunza na kufanya marekebisho yanayohitajika kutokana na hatua hiyo, na kuvumbua na kufanya mabadiliko chanya muda unavyosonga.

**Uimarishaji Uwezo wa Wazawa** ni uwekezaji wa kimkakati na makusudi katika mchakato wa kushirikiana na wadau kutoka katika sekta mbalimbali—watu, mashirika na mitandao—ili kwa pamoja kuboresha utendaji wa mfumo wa kizawa ili kuzalisha matokeo yanayothaminiwa katika eneo husika na ya maendeleo endelevu.

Zaidi ya hayo, katika uwanja wa kibinadamu na maendeleo ya kimataifa, makubaliano yameibuka kuhusu umuhimu wa uimarishaji wa uwezo—ambao ni wa pamoja na unaoongozwa na wazawa—katika kuchangia maendeleo endelevu. Hata hivyo, licha ya makubaliano haya yaliyoibuka, USAID haijawahi kuwa na sera kuu na ya pamoja kama Shirika kuhusu Kuimarisha Uwezo wa Wazawa. Sera hii inaziba pengo hilo na kuthibitishia uongozi wa kimataifa wa USAID kwa kulipatia Shirika maono ya uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa yanayojikita katika makubaliano ya uwanja wa maendeleo, maoni kutoka kwa wahusika na washirika wazawa, na uzoefu wa miaka mingi wa utekelezaji na ushahidi. Maono haya mapya yatajikita katika kujitolea kwa ushirikiano unaozingatia kuheshimiana na kutendeana na ambapo maoni ya wadau kutoka katika sekta mbalimbali kutoka asili na tamaduni zote yatathaminiwa, kutumia uwezo wao wa kipekee na kuongoza maendeleo ya nchi yao.

Usaidizi wa USAID katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa lazima upangwe kwa njia ambayo hutumia uwezo uliopo wa wahusika na mifumo ya kizawa, kushughulikia mazingira anuwai ya nchi na kikanda na kufungamana na vipaumbele vya kimkakati vya USAID. Hii inamaanisha kwamba mbinu za Kuimarisha Uwezo wa Wazawa zitatofautiana. Ili kuwezesha utekelezaji wenye uwiano wa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa katika sekta na mazingira anuwai, Sera ya USAID ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa inaasisi maono ya Shirika zima kulingana na kujitolea kwa pamoja kwa seti ya kanuni ambazo zitaongoza mipango yote husika ya USAID ya usaidizi wa kibinadamu na maendeleo.

Sera hii inapanga kanuni saba zinazoimarishana kwa pamoja za uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa katika mada mbili: mipango yenye ufanisi na ubia wenye usawa.

**Kanuni za mipango yenye ufanisi ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa**, ambazo zimeelezwa katika Sehemu ya Pili, huelekeza uelewa wetu kuhusu sababu na ni katika hali zipi ambapo maamuzi ya kimkakati na makusudi ambayo huimarisha uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali kama sehemu ya Mzunguko wa Mpango wa USAID yanaweza kuchangia katika mabadiliko mapana ya mifumo na matokeo endelevu. Kanuni hizi pia huelekeza uelewa wetu kuhusu kwanini kupima utendaji ni muhimu.

**Kanuni za ubia wenye usawa katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa**, ambazo zimewasilishwa katika Sehemu ya Tatu, huelekeza jinsi mipango ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa katika sekta na kanda tofauti utafadhiliwa kupitia ubia unaozingatia kuheshimiana na kutendeana.

Kwa pamoja, kanuni hizi, zinazotokana na msingi thabiti wa ushahidi na mchakato mpana wa mashauriano ambapo USAID ilitoa kipaumbele kwa ushirikishaji na maoni ya wahusika na mashirika ya ndani (yameelezwa katika Ripoti ya Maoni ya Umma), zitaongoza USAID katika kufanya maamuzi ya kimkakati na makusudi ili kuwezesha mipango ya uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa kupitia ubia wenye usawa. Zaidi ya hayo, kwa sababu uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa unahitaji kudhamiria, rasilimali, na upeo mrefu wa muda, sera inahitimisha kwa jinsi USAID inavyopanga kutekeleza kanuni zilizofafanuliwa humu. Sehemu ya Nne inaeleza mchakato wa udhibiti wa mabadiliko na muundo utakaoongoza utekelezaji wenye ufanisi wa sera.

## KANUNI ZA MIPANGO YENYE UFANISI YA KUIMARISHA UWEZO WA WAZAWA

1. Anza kwa mfumo wa ndani.
2. Imarisha uwezo anuwai kupitia mbinu anuwai.
3. Panga na upime maboresho ya utendaji ukishirikiana na washirika wazawa.

## KANUNI ZA UBIA WENYE USAWA KATIKA KUIMARISHA UWEZO WA WAZAWA

4. Fungamanisha uimarishaji wa uwezo na vipaumbele vya wazawa.
5. Tambua vyema na kutumia uwezo uliopo.
6. Zingatia na kupunguza athari zisizokusudiwa za uwezeshaji wetu wa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa.
7. Dumisha ushirikiano na washirika wazawa.



# I. MAONO YA PAMOJA YA KUIMARISHA UWEZO WA WAZAWA

> "Kupitia sera hii, USAID inanuia kuweka maono mapya ya uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa yanayojikita kwa makubaliano ya uwanja wa maendeleo, maoni kutoka kwa wahusika na washirika wa ndani, na uzoefu wa miaka mingi wa utekelezaji na ushahidi."

Maendeleo endelevu yanategemea wadau kutoka katika sekta mbalimbali kuongoza juhudi za kuboresha jamii zao na kufanya kazi kwa umoja na pamoja ili kutimiza malengo ya juhudi hizo. Kwa sababu hii, Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kumekuwa na kumeendelea kuwa kipengele cha msingi cha mipango ya USAID. Uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa unaweza kupelekea ukuaji wa kiuchumi wa pamoja; maendeleo ya mapema ya huduma muhimu za afya, chakula na lishe, na huduma na mifumo ya elimu; na kukuza utawala wa kidemokrasia. Kuimarisha Uwezo wa Wazawa pia kunaweza kushughulikia sababu zilizopo za udhaifu, kuimarisha mifumo ya ndani ya kuhudumia matukio ya kibinadamu, na kuongeza ustahimilivu dhidi ya mishtuko na mifadhaiko. Kutokana na hilo, uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa husaidia nchi kuzuia, kupunguza na kupata ahueni baada ya migogoro. Hatimaye, uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali ni kigezo muhimu cha mafanikio ya USAID na washirika wake katika kufikia na kudumisha mafanikio ya kibinadamu na maendeleo duniani kote.

Zaidi ya hayo, katika uwanda wa kibinadamu na maendeleo ya kimataifa, makubaliano yameibuka kuhusu umuhimu wa uimarishaji wa uwezo—ambao ni wa pamoja na unaoongozwa na wenyeji—katika kuchangia maendeleo endelevu. Ahadi za kiwango cha juu za mashirika ya kimataifa ya maendeleo, wafadhili na serikali, ikiwemo zilizotolewa katika mikutano ya kimataifa ya ufanisi wa misaada huko Paris, Accra na Busan na kuungwa mkono kupitia mikataba ya kimataifa kama vile Mapatano Makuu na Maendeleo Endelevu (Grand Bargain and Sustainable Development Goals, SDGs), zimesisitiza umuhimu wa uwezo wa kitaifa na umiliki wa ndani katika kufikia maendeleo endelevu. wadau kutoka katika sekta mbalimbali, washirika wa kimataifa na Wafanyakazi wa USAID Walioajiriwa Katika Eneo Husika, ambao wote wana majukumu muhimu katika mfumo wa ndani, pia wamethibitisha umuhimu wa uwezo wa kitaifa na umiliki wa ndani. Mashauriano ya kuelekeza sera hii yalidhihirisha

Picha kwa Hisani ya: Bobby Neptune kwa ajili ya USAID

## MAONO YA SERA

USAID hufanya maamuzi ya kimkakati na makusudi ya kwanini na jinsi ya kuwekeza katika uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali kulingana na uelewa wa pamoja wa kanuni za uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo kwa wazawa.

makubaliano kwamba mbinu za uimarishaji uwezo zinazoongozwa na wenyeji huwasaidia watu, mashirika na mitandao ya ndani kuhudumia jamii zao vyema zaidi, kushughulikia hali za migogoro kwa ufanisi zaidi, kukuza ustadi maalum, kukusanya rasilimali, kushawishi sera, kupata usaidizi wa kibinadamu na matokeo ya maendeleo ya pamoja zaidi, na hatimaye kumaliza hitaji la ufadhili wa wafadhili wa kimataifa.

Zaidi ya hayo, ushahidi na uzoefu unaonesha kwamba uwezeshaji wa uimarishaji wa uwezo unaweza kuwa na athari isiyotarajiwa ya kuongeza mizigo ya muda na rasilimali kwa wadau kutoka katika sekta mbalimbali, uwezeshaji huu unapoelekezwa na kutekelezwa bila kuzingatia mfumo wa ndani au maslahi ya wadau kutoka katika sekta mbalimbali. Mifano ya hili ni pamoja na kuwaomba wadau kutoka katika sekta mbalimbali: kuhudumu kama waratibu wa usimamizi na ugavi ili kuwahudumia wahusika wa kimataifa; kushughulikia masharti tofauti ya kuhakikisha utiifu kwa sheria kwa ajili ya wafadhili mbalimbali wa kimataifa; na kuunda mifumo sambamba ya ziada ya utendakazi kama vile udhibiti na kutoa ripoti za kifedha. Hatimaye, mahitaji haya ya muda na rasilimali hupunguza thamani ya matokeo ya maendeleo endelevu yanayoongozwa na wenyeji na kuzidisha ukosefu wa usawa duniani.

Licha ya makubaliano na ushahidi unaojitokeza kuhusu sifa kuu ya uimarishaji wa pamoja wa uwezo na unaoongozwa na wenyeji, USAID haijawahi kuwa na sera kuu na ya pamoja ya Shirika kuhusu Kuimarisha Uwezo wa Wazawa. Kupitia sera hii, USAID inanuia kuweka maono mapya ya uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo kwa wazawa yanayojikita katika makubaliano ya uwanja wa maendeleo, maoni kutoka kwa wahusika na washirika wa ndani, na uzoefu wa miaka mingi wa utekelezaji na ushahidi.

Maono haya mapya yamejikita katika kujitolea kwa ushirikiano unaotokana na kuheshimiana na kutendeana na ambapo maoni ya wadau kutoka katika sekta mbalimbali kutoka asili na tamaduni zote yatathaminiwa, kutumia uwezo wao wa kipekee na kuongoza maendeleo ya nchi yao. Kuwezesha maono haya mapya kutatuhitaji kutafuta makusudi mawazo kutoka kwa wale ambao huenda hawana ufikiaji kwa ulinzi wa kisheria au ushiriki wa kijamii na kiuchumi kutokana na utambulisho wao. Lazima pia tuchukue hatua zaidi ili kupunguza makusudi mzigo wa muda na rasilimali kwa wadau kutoka katika sekta mbalimbali wanaotafuta msaada wetu katika uimarishaji wa uwezo. Kwa kufanya hivyo, USAID ina nafasi nzuri ya kuakisi kanuni za maendeleo ya pamoja katika mipango yetu yote ya kuimarisha uwezo na kushirikisha wadau kutoka katika sekta mbalimbali katika ushirikiano thabiti na wenye usawa zaidi katika shughuli za kuimarisha uwezo.

Madhumuni ya sera hii ni kuasisi maono ya Shirika zima ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kulingana na kujitolea kwa pamoja kwa seti ya kanuni ambazo zitaongoza mipango inayohusika ya USAID ya misaada ya kibinadamu na maendeleo. Uungaji mkono wa USAID kwa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa lazima upangwe kwa njia ambayo hutumia uwezo uliopo wa wahusika na mifumo ya ndani, kushughulikia mazingira anuwai ya nchi na kikanda na kufungamana na vipaumbele vya kimkakati vya USAID. Hii inamaanisha kwamba mbinu za Kuimarisha Uwezo wa Wazawa zitatofautiana. Hivyo, ili kutekeleza Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kwa uwiano katika sekta na mazingira anuwai, USAID inapitisha seti ya kanuni za pamoja ambazo zitasaidia kwa usawa wadau kutoka katika sekta mbalimbali kumiliki na kusimamia maendeleo yao wenyewe.

Kanuni si sheria wala maadili. Kinyume na sheria, kanuni zinaweza kubadilika ili kulingana na hali husika na huwezesha uwiano bila kushurutisha. Kinyume na maadili, kanuni hulenga vitendo na kuongoza maamuzi na uchaguzi. Kanuni zinaweza kusaidia USAID kutafsiri maadili yake—shauku kwa dhamira, ubora, uadilifu, heshima, uwezeshaji, ujumuishaji na utayari wa kujifunza— kuwa tabia. Nia yetu ni kwamba kanuni zilizoelezwa kote katika sera hii zitaelekeza kwa urahisi na kwa pamoja utekelezaji wa mipango yote ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa inayofadhiliwa na USAID. Sera hii inapanga kanuni saba zinazoimarishana kwa pamoja za uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa katika mada mbili: mipango yenye ufanisi na ubia wenye usawa.

**Kanuni za mipango yenye ufanisi ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa**, ambazo zimeelezwa katika Sehemu ya Pili, huelekeza uelewa wetu wa kwanini na ni katika hali zipi ambapo maamuzi ya kimkakati na makusudi ambayo huimarisha uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali—kama sehemu ya Mzunguko wa Mpango wa USAID—yanaweza kuchangia katika mabadiliko mapana ya mifumo na matokeo endelevu. Kanuni hizi pia huelekeza uelewa wetu kuhusu kwa nini kupima utendaji ni muhimu.

**Kanuni za ubia wenye usawa katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa**, ambazo zimewasilishwa katika Sehemu ya Tatu, huelekeza jinsi mipango ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa katika sekta na kanda tofauti itafadhiliwa kwa ubia unaotokana na kuheshimiana na kutendeana.

Msingi thabiti wa ushahidi na mchakato mpana wa mashauriano ambapo USAID ilitoa kipaumbele kwa ushirikishaji na maoni ya wahusika na mashirika ya ndani (yameelezwa katika Ripoti ya Maoni ya Umma) hupelekea kanuni saba za uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa ambazo zimeelezwa katika Sehemu za II na III. Zaidi ya hayo, kwa sababu uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa unahitaji kudhamiria, rasilimali, na upeo mrefu wa muda, sera inahitimisha kwa jinsi USAID inavyopanga kutekeleza kanuni zilizofafanuliwa humu. Sehemu ya Nne inaeleza mchakato wa udhibiti wa mabadiliko na muundo wa kuongoza utekelezaji wenye ufanisi wa sera.



Picha kwa Hisani ya: Jamie Barnett/FHI 360




# II. KANUNI ZA MIPANGO YENYE UFANISI YA KUIMARISHA UWEZO WA WAZAWA

Kushirikiana na wadau kutoka katika sekta mbalimbali ili kuimarisha uwezo wao ni mojawapo ya njia zenye ufanisi zaidi za kuendeleza maendeleo endelevu. Hata hivyo, Kuimarisha Uwezo wa Wazawa hauleti moja kwa moja utendaji ulioboreka na maendeleo endelevu, wala kuimarisha uwezo siku zote sio uingiliaji kati wa lazima au uingiliaji wa kiprogramu unaohitajika. USAID inapaswa kukabiliana na kila changamoto au mazingira kwa kutambua kuwa wadau kutoka katika sekta mbalimbali wana uwezo mwingi unaohitajika ili kuleta maendeleo endelevu lakini pia wanaweza kutaka usaidizi unaoambatana. Watu waliomo na wanaoathiriwa na mifumo ya ndani tunamofanyia kazi wanapaswa kuongoza uamuzi wetu wa kuwekeza katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa na matarajio yetu ya aina za kuboreka kwa utendaji ambazo mipango yetu inaweza kuchochea na kuwezesha.

> "Hii inamaanisha kwamba uimarishaji wenye ufanisi na endelevu wa uwezo wa ndani unahitaji 'jambo linalofaa zaidi'—sio 'kitendo bora zaidi'—mbinu ambayo imeundwa kulingana na mfumo wa ndani."

Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kuna uwezekano mkubwa wa kuchangia katika kupatikana kwa matokeo endelevu wakati uamuzi wa kuwekeza katika uimarishaji wa uwezo unapofanywa kwa ushirikiano na washirika wa ndani na kutokana na uelewa wa kina na wa pamoja wa uhusiano kati ya uwezo na mabadiliko endelevu katika ngazi ya mifumo. Zaidi ya hayo, kuimarisha uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali ni muhimu tu katika mazingira ya jinsi mfumo wa ndani hufanya kazi na jinsi wahusika waliowekwa ndani ya mfumo huo hutekeleza majukumu yao na kuingiliana wao kwa wao, sheria za mfumo, na rasilimali zilizopo ndani ya mfumo huo. Hii inamaanisha kwamba uimarishaji wenye ufanisi na endelevu wa uwezo wa wazawa unahitaji "jambo linalofaa zaidi"—sio "kitendo bora zaidi"—mbinu ambayo imeundwa kulingana na mfumo wa ndani. Kwa hivyo, kabla ya USAID kujitolea kwa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa, lazima tuelewe uhusiano kati ya uwezo wa ndani na maendeleo endelevu. Uelewa huu lazima ujikite katika uchanganuzi wa mfumo wa ndani, wahusika katika mfumo wa ndani, na uwezo wao uliopo, mahusiano na vipaumbele. Lazima pia tuzingatie njia mbalimbali ambazo USAID inaweza kutumia uwezo wake mkubwa kuwezesha maendeleo endelevu na kupima mafanikio yake.

Kutokana na hilo, USAID imejitolea kwenye kanuni tatu za mipango ya uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa, kama ilivyoelezwa katika sehemu hii: anza kwa mfumo wa ndani, imarisha uwezo anuwai kupitia mbinu anuwai, na panga na upime maboresho ya utendaji ukishirikiana na washirika wazawa. Kanuni hizi tatu zitaelekeza uelewa wetu wa kwanini na ni katika hali zipi kuimarisha uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali—kama sehemu ya Mzunguko wa Mpango wa USAID—kunaweza kuchangia katika mabadiliko mapana ya mifumo na matokeo ya maendeleo endelevu. Kanuni hizi pia huelekeza uelewa wetu kuhusu kwa nini kupima utendaji ni muhimu.

Picha kwa Hisani ya: USAID/Ufilipino

## Kanuni ya 1: Anza kwa mfumo wa kizawa.

Wadau kutoka katika sekta mbalimbali—watu binafsi, mashirika na mitandao—ndiyo waleta mabadiliko muhimu zaidi katika jumuiya na jamii zao. Uwekezaji wa USAID katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa lazima ulenge kuwasaidia wadau kutoka katika sekta mbalimbali kutekeleza vyema zaidi kazi muhimu katika kupata mabadiliko chanya na endelevu katika ngazi ya mfumo. Katika utendaji halisi, hili huanza kwa kuelewa mfumo wa kizawa. Kuelewa mfumo wa kizawa[1] huelekeza kwanini na ni katika hali zipi Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kunaweza kuchangia katika mabadiliko chanya na endelevu zaidi katika ngazi ya mfumo.

Kujifunza kuhusu mfumo wa kizawa lazima kuwe zaidi ya kukusanya habari kutoka kwa upande mmoja. Kwa kushirikiana na wadau kutoka katika sekta mbalimbali, na kutumia maarifa na ustadi wa Wafanyakazi wa USAID Walioajiriwa Katika Eneo Husika, lazima tuelewe jinsi mfumo wa kizawa unavyofanya kazi, umahiri na uwezo wake kiutendaji uliopo, mienendo na mahusiano kati ya wahusika, na sheria, motisha na kaida za mazingira ambamo wahusika wapo. Kupata uelewa pamoja—wakati kikundi cha watu walio na asili tofauti kinapoelewa hali au taarifa pana, changamano na zinazobadilika—kunaweza kusaidia USAID kuepuka maeneo yasiyoeleweka, kuboresha uvumbuzi na ubunifu, na kupelekea matokeo endelevu zaidi ya maendeleo. Hata hivyo, ili kupata manufaa kamili kutokana na kupata uelewa pamoja, USAID na washirika wake lazima wajumuishe kikamilifu na makusudi watu kutoka kwa makundi yaliyotengwa na yenye uwakilishi mdogo, ambayo yanaweza kujumuisha lakini sio tu, wanawake na wasichana, watu wenye ulemavu, mashoga, wakimbizi, wahamiaji, Watu wa Kabila Asili, vijana na wazee, vikundi vya kidini vya watu wachache, vikundi vya rangi na makabila ya watu wachache, watu wa matabaka ya chini na watu wenye mahitaji ya afya ya akili. Ikiwa hatutajumuisha kwa makusudi maoni ya wahusika wanaowakilisha makundi haya, tunahatarisha kuwatenga bila kukusudia.

1 Kwa ufafanuzi mpana zaidi wa mifumo ya ndani, rejelea Sera ya USAID ya Utaratibu wa Mifumo ya Ndani ya USAID. "Local Systems (Mifumo ya Ndani): A Framework For Supporting Sustained Development (Mfumo Wa Kuwezesha Maendeleo Endelevu)" (Aprili 2014): https://www.usaid.gov/policy/local-systems-framework

USAID inatambua tofauti za uwezo wa wazawa uliopo katika nchi washirika wetu na inabadilisha makusudi matumizi yake ya istilahi kutoka "kukuza uwezo" au "kustawisha uwezo" hadi "kuimarisha uwezo." Zaidi ya hayo, uwezo wa mhusika yeyote unategemea mno kufaa kwake ndani ya muktadha na mazingira wezeshi ya mfumo wa ndani.

Unavyoeleweka na kutumiwa na USAID, **uwezo** unajumuisha maarifa, ujuzi, na motisha pamoja na mahusiano yanayomwezesha mhusika—mtu, shirika au mtandao—kuchukua hatua ili kubuni na kutekeleza masuluhisho ya changamoto za ndani za maendeleo, kujifunza na kufanya marekebisho yanayohitajika kutokana na hatua hiyo, na kuvumbua na kufanya mabadiliko chanya muda unavyosonga.

**Kuimarisha Uwezo wa Wazawa** ni uwekezaji wa kimkakati na makusudi katika mchakato wa kushirikiana na wadau kutoka katika sekta mbalimbali—watu, mashirika na mitandao—ili kwa pamoja kuboresha utendaji wa mfumo wa kizawa ili kuzalisha matokeo yanayothaminiwa katika eneo husika na ya maendeleo endelevu.

Mbinu moja ya kuelewa mifumo ya kizawa na kubainisha ikiwa uwekezaji katika kuimarisha uwezo wa wahusika wakuu wa ndani unaweza kuchangia kwa ufanisi katika mabadiliko endelevu katika ngazi ya mfumo ni kuwasikiliza wadau kutoka katika sekta mbalimbali kuhusu **majukumu** ya sasa na yanayotarajiwa wanayotekeleza na **mahusiano** waliyo nayo na wanayotaka, pamoja na **sheria** zisizo rasmi na zilizo rasmi na **rasilimali** zinazowezesha au kukwaza uwezo wao wa kufikia **matokeo** wanayotaka. Katika kila mfumo wa ndani, watu huwa na majukumu mengi—ya kitamaduni, yanayotofautishwa kijamii, yanayolingana na hali mahususi, ya kijamii na kibayolojia, au yanayolingana na jinsia—kila siku. Na maingiliano ya wahusika tofauti, kulingana na majukumu mbalimbali wanayotekeleza, hupelekea taratibu na mahusiano ambayo hubuni muundo wa taasisi na jamii. Hivyo, uungaji mkono wa USAID wa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa utafanikiwa zaidi tunapofanya mambo kimkakati na makusudi ili kuwasaidia wahusika wakuu kutekeleza majukumu na kuwa na mahusiano ambayo huwasaidia kuchochea na kudumisha mabadiliko chanya wanayothamini na kuona kuwa muhimu

katika jumuiya na jamii zao. Uzingatiaji unaofuata kuhusu majukumu, mahusiano, sheria na rasilimali unaweza kusaidia kuelekeza kufanya maamuzi ya kimkakati kuhusu iwapo na ni katika hali zipi uwekezaji katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa unaweza kuwa na ufanisi zaidi.

**Majukumu na mahusiano:**
Matokeo ya maendeleo hutokana na vitendo na maingiliano ya aina tofauti za wahusika. Katika hali nyingi, aina nyingi za wahusika huchangia jinsi ambavyo mfumo wa kizawa hufanya kazi (au kutenda). Hivyo, lazima tuelewe kiwango na tofauti za wahusika na majukumu ya kipekee wanayofanya ndani ya mfumo, kabla ya kuamua ikiwa kuimarisha uwezo wa wahusika teule ili kutekeleza majukumu ambayo yanaweza kuathiri mabadiliko ya ngazi ya mifumo kunahitajika. Zaidi ya hayo, kwa sababu matokeo na umiliki wa masuluhisho hutokana na maingiliano ya wahusika wengi, kupanua lengo letu kuwa zaidi ya kuimarisha uwezo wa mhusika mmoja kunaweza kuwa na uwezekano mkubwa wa kuboresha utendaji kazi wa jumla wa mfumo. Mipango ya USAID lazima izingatie na inapaswa kutoa kipaumbele kwa fursa za kuwezesha matokeo ya pamoja kupitia uimarishaji wa mtandao.

**Majukumu na rasilimali:**
Kabla ya kuamua ikiwa uwekezaji katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa unaweza kupelekea uboreshaji wa kiutendaji, lazima pia tuzingatie vipengele vingine vya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kimazingira katika mfumo wa kizawa ambavyo vinaweza kushawishi na kuhamasisha mabadiliko chanya na endelevu katika ngazi ya mifumo. Katika mifumo ya kizawa ambapo kuna mazoea ya kutengwa kijamii kulingana na utambulisho, imani za kitamaduni au kaida nyingine za kijamii, baadhi ya wadau kutoka katika sekta mbalimbali wanaweza kupinga mabadiliko ya hali iliyopo. Mahusiano yasiyo na usawa wa mamlaka pia yanaweza kuzuia ufikiaji wa rasilimali zinazohitajika ili kuchochea mabadiliko ya kijamii. Katika hali hizi, uwekezaji unaofanywa ili tu kuimarisha uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali huenda usiwe wa kutosha kuchochea mabadiliko endelevu na unaweza kuhitaji kuunganishwa na juhudi nyingine za kuimarisha mifumo ya kizawa. Hivyo, pia tunaweza kuhitaji kuwasaidia wadau kutoka katika sekta mbalimbali kutambua njia za kupata rasilimali za kifedha, kupata ufikiaji kwa au kutumia rasilimali nyingine au kuhimiza utekelezaji wa sera ili mfumo ufanye kazi vyema zaidi.

Kwa ujumla, uwekezaji katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa pekee hautatosha kufikia matokeo ya maendeleo endelevu. Huku ikishirikiana na wadau kutoka katika sekta mbalimbali, USAID inapaswa kwanza kuchanganua mfumo wa ndani na kutafakari kuhusu uwezo wa ndani uliopo, aina ya usaidizi wa kuimarisha uwezo ambao wadau kutoka katika sekta mbalimbali wanataka na wanahitaji, na ni mbinu zipi nyingine za mipango zinaweza kuhitajika pamoja na juhudi za Kuimarisha Uwezo wa Wazawa ili kufikia matokeo ya maendeleo endelevu. Hapo tu ndipo tunaweza kusonga mbele kwa ujasiri na kufanya maamuzi ya kimkakati na makusudi kuhusu jinsi ya kuwekeza katika mbinu ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa.

### KUANGAZIA MBINU YA KUIMARISHA UWEZO WA WAZAWA: MFUMO WA R5

Mfumo wa R5 ni zana inayotekelezeka ya kuhimiza utendaji bora wa mifumo. Unaangazia sehemu tano kuu za mifumo: Results (Matokeo), Roles (Majukumu), Relationships (Mahusiano), Rules (Sheria) na Resources (Rasilimali). Kwa pamoja, R5 hizi zinaweza kutumika kama lenzi za kuelewa mifumo ya kizawa na kama mwongozo wa kufanya uamuzi kuhusu iwapo tutawekeza, pamoja na kuchagua na kufuatilia, uingiliaji kati wa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa unaokusudiwa kuchangia mabadiliko chanya na endelevu zaidi katika ngazi ya mfumo. Kwa pamoja, R5 hizi huakisi sehemu za msingi za mfumo.

Dhana muhimu ya Mifumo ya R5 ni kwamba uendelevu unategemea uwezo wa mfumo wa kizawa kutoa matokeo yanayothaminiwa ya maendeleo muda unavyosonga. Kutumia Mfumo wa R5 katika mchakato wa kubuni mpango husaidia USAID kuhakikisha kwamba uteuzi wa uingiliaji kati wa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa unaongozwa na mazingira ya ndani na una uwezekano mkubwa wa kuwasaidia wadau kutoka katika sekta mbalimbali kutekeleza majukumu na kubuni mahusiano ya kushawishi mfumo kutoa matokeo yanayothaminiwa ambayo yanadumishwa muda unavyosonga.

NYENZO: The 5Rs in the Program Cycle (R5 katika Mzunguko wa Mpango)

# TAARIFA KUHUSU MAJUKUMU NA MAHUSIANO

Ilivyofafanuliwa katika sera ya USAID, Mifumo ya Kizawa: Mfumo wa Kuwezesha Maendeleo Endelevu, mfumo wa kizawa unajumuisha seti ya wahusika waliounganishwa ambao kwa pamoja hupelekea matokeo maalum ya maendeleo. Katika mfumo wowote wa kizawa, kupata na kudumisha matokeo yoyote ya maendeleo kunategemea michango ya wahusika wengi na waliounganishwa. Wahusika hawa wanaweza kuakisi viwango tofauti vya kijamii (k.m., watu, mashirika au mitandao) na kufanya kazi au kwenye viwango tofauti vya kijiografia (k.m., eneo dogo la kitaifa, kitaifa au kikanda).

Baadhi ya wahusika wanaweza kuwa wenyeji katika mfumo wa kizawa, huku wengine huenda wakatokea nje ya nchi. Bila kujali hilo, ni kujitolea kwao katika kutumia mamlaka yao miongoni mwao wenyewe na wajibu wao wa pamoja wa kupambana na changamoto ya pamoja ya maendeleo kunakowaunganisha pamoja kama mfumo wa kizawa.


Changamoto zinazokabili ulimwengu leo zinahitaji ubunifu, uwezo na mawazo bunifu ya watu na mashirika ulimwenguni kote. Katika sera hii, USAID inatumia ufafanuzi unaofuata kurejelea baadhi tu ya wahusika ambao ni sehemu ya mifumo ya kizawa.

- **Wadau kutoka katika sekta mbalimbali** ni watu, mashirika na mitandao iliyoanzilishwa na inayoongozwa na watu ndani ya nchi au eneo maalum, ikijumuisha serikali katika ngazi za kitaifa na eneo dogo la kitaifa.


- **Washirika wazawa** ni watu, mashirika na mitandao iliyoanzishwa na inayoongozwa na watu ndani ya nchi au eneo maalum, ikijumuisha serikali katika ngazi za kitaifa na eneo dogo la kitaifa wakati wanashirikiana na USAID kama wakandarasi wa moja kwa moja au wapokeaji au kama wanufaishwa wadogo, iwe kupitia ununuzi au usaidizi.

- **Washirika wa kimataifa** ni mashirika ya kimataifa yasiyo ya kiserikali (INGOs), kampuni za kimataifa za sekta ya binafsi na mashirika mengine ya kimataifa yanaposhirikiana na USAID kama wakandarasi wa moja kwa moja au wapokeaji au kama wanufaishwa wadogo, iwe kupitia ununuzi au usaidizi.

**Mbinu ya Hatua kwa Hatua ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa**




**Mbinu ya Mtandao ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa**



- **Wafadhili wengine wa kimataifa** ni mashirika ya kimataifa yasiyo ya kiserikali, kampuni za kimataifa za sekta binafsi na mashirika mengine ya kimataifa yanapotoa usaidizi wa maendeleo yenyewe.

Kila mojawapo ya aina hizi za wahusika inaweza kuchangia uwezo na rasilimali tofauti katika kutatua changamoto za maendeleo kimataifa. Hata hivyo, kufikia maono ya sera hii na kuendeleza usawa na ushirikishaji wa kimataifa kunaweza kuhitaji baadhi ya wahusika kubadilisha majukumu yao katika mipango ya kibinadamu na maendeleo katika mifumo ya kizawa. USAID, wafadhili wengine wa kimataifa na washirika wa kimataifa wanapohudumu kama wawezeshaji, waratibu na wahamasishaji na kuwasaidia wadau kutoka katika sekta mbalimbali na washirika wa ndani kuongoza katika sehemu kuu ya mbinu za upangaji na utekelezaji wa mtandao, kama inavyooneshwa hapa chini, mipango ya USAID inaweza kuhamisha uwezo wa kuweka ajenda na kufanya maamuzi hadi kwa watu wanaoathiriwa moja kwa moja na mipango ya misaada na maendeleo.


## 2 Kanuni ya 2: Imarisha uwezo anuwai kupitia mbinu anuwai.

Mara tu USAID inapopata uelewa wa kina wa mfumo wa kizawa na kuamua kwa pamoja na washirika wazawa kuwekeza katika uimarishaji wa uwezo, tunaweza kuamua mbinu inayofaa zaidi. Kuimarisha uwezo kwa mafanikio huwasaidia wadau kutoka katika sekta mbalimbali kutimiza majukumu na kuwa na mahusiano yatakayobuni muundo wa mfumo wa kizawa kwa njia ambayo inakidhi matamanio, malengo na mahitaji yao. Kwa hivyo, katika kuchagua mbinu, lazima tushirikiane na wahusika wazawa ili kuelewa vipaumbele vyao, uwezo uliopo na malengo ya kuboresha utendaji. Lazima pia tutambue kwamba kila mhusika ni tofauti, hukua kwa njia za kipekee na ana viwango tofauti vya uwezo wa kufanya mambo, mamlaka na ufikiaji wa rasilimali. Lazima tuepuke mbinu inayotumia utaratibu mmoja kwa wote na kuweza kufanya marekebisho inapohitajika, kuwa wabunifu na kuvumbua njia mpya tunapotumia mbinu tofauti ili kukidhi mahitaji mbalimbali ya wadau kutoka katika sekta mbalimbali na malengo ya muda mrefu ya kuimarisha mifumo ya kizawa. Uzingatiaji unaofuata kuhusu kinachofaa kwa mfumo wa kizawa na jukumu la USAID unaweza kusaidia kuelekeza kufanya maamuzi ya kimkakati kuhusu kwanini na ni katika hali zipi mbinu tofauti za Kuimarisha Uwezo wa Wazawa zinaweza kuwa na ufanisi zaidi.

**Kinachofaa kwa mfumo wa kizawa:**
Uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa hufanya mambo kimkakati na makusudi kuhusu wahusika wa kushirikisha na jinsi ya kuwasaidia. Huzingatia ngazi ya kijamii (yaani, ngazi ya mtu binafsi, shirika au mtandao) na upana wa kijiografia (yaani, upana wa eneo dogo la kitaifa, kitaifa, kikanda au kiulimwengu) cha wadau kutoka katika sekta mbalimbali kuhusiana na malengo ya maendeleo. Pia huzingatia kwamba aina nyingi za uwezo na mbinu zinaweza kuhitajika ili kuboresha utendaji wa muda mfupi na muda mrefu wa wahusika na mifumo ya kizawa. Baadhi ya usimamizi wa kiufundi na uwezo wa kifedha humsaidia mhusika kutoa bidhaa au huduma au kutekeleza majukumu mahususi vyema zaidi, kama vile kufanya na kudumisha utafiti wa kina au mpango wa matibabu unaofadhiliwa. Uwezo mwingine wa kiutendaji au kimahusiano humsaidia mhusika kutafakari na kuwajibikia maoni ya jamii, kuhudumu na kuongoza kama kiongozi anayewajibika, kutatua matatizo na kufanya marekebisho ili kusalia kuwa muhimu, au kuunda ushirikiano mpya ili kushawishi matumizi ya ujuzi na rasilimali za pamoja. Bila kujali aina ya uwezo, USAID itajitahidi kuimarisha uwezo wa wazawa kwa njia ambazo zinafanya zaidi ya kutoa matokeo ya muda mfupi na kushawishi matumizi ya uwezo mbalimbali katika kufikia matokeo ya muda mrefu.

Mara nyingi sana, huwa tunateua mbinu inayotegemea kutoa mafunzo ili kuimarisha uwezo kwa sababu inaweza kutabirika na huonekana dhahiri. Hata hivyo, mafunzo mara

## Mbinu za Kuimarisha Uwezo Hutofautiana Katika Ngazi za Kijamii




**Mifumo ya Kizawa.** Mfumo wa ndani hufanya kazi vyema wakati watu, mashirika na mitandao yake ina uwezo wa kutekeleza majukumu na kubuni mahusiano yanayoiwezesha kuzalisha na kuendeleza kwa pamoja masuluhisho yanayothaminiwa katika eneo husika ya changamoto za kibinadamu na maendeleo.

**Mitandao**. Katika ngazi ya mtandao, mbinu zenye ufanisi za kuimarisha uwezo huwezesha na kuunga mkono uwezo wa wahusika wengi kuratibu, kushirikiana na kufanya kazi pamoja ili kufikia matokeo ya pamoja.

**Mashirika**. Uimarishaji wa uwezo wa mashirika husaidia mashirika, kikundi cha watu wanaofanya kazi pamoja kwa njia iliyopangwa kwa madhumuni ya pamoja, kufikia matamanio yao ya kimkakati na kutoa matokeo kwa wadau wanaowahudumia. Uwezo wa mashirika unaohusiana na mifumo ya binadamu, halisi, ya kifedha na ya kiteknolojia hutegemeana. Inapaswa kuangaziwa kama iliyo muhimu katika kuwezesha michango ya mashirika kwa maendeleo endelevu.

**Watu**. Katika ngazi ya mtu, mbinu za kujifunza kwa watu wazima zinazofaa kitamaduni hupelekea kuthamini kujifunza kwa maisha yote. Mbinu hizi hutoa mazingira salama ya kujifunzia, heshima kwa wanafunzi na fursa za kutumia maarifa mapya, ujuzi au mitazamo mara moja na kisha kufikiria kuhusu utendaji huo mpya.

nyingi huwa na mitindo ya mawazo ambapo jambo moja huchukuliwa kufaa kwa wote kuhusu jinsi wadau kutoka katika sekta mbalimbali wanapaswa kuonekana na mara nyingi hutanguliza ujuzi wa nje kuliko ujuzi wa kizawa.

Kiukweli, mbinu mbalimbali za kuimarisha uwezo zinaweza kuhitajika ili kuwasaidia wadau kutoka katika sekta mbalimbali kufikia malengo yao ya utendaji na kuchangia mabadiliko chanya katika jumuiya na jamii zao. Kwa hivyo, mbinu zinapaswa kuwa zinazofaa kwa madhumuni na kuundwa pamoja na wadau kutoka katika sekta mbalimbali, kwa kuzingatia matamanio, malengo na mahitaji ya kila mhusika mzawa na sheria na rasilimali za mfumo wa kizawa. Mbinu zinaweza kujumuisha kuandamana na wadau kutoka katika sekta mbalimbali kujifunza kwa kufanya kupitia mbinu za ushiriki, kuunda fursa za kujifunza kati ya wenza na kuwezesha udalali wa mahusiano na kuimarisha mtandao. Katika baadhi ya hali, mafunzo yanaweza kuwa na ufanisi lakini hayapaswi kuwa mbinu yetu chaguomsingi ya kuimarisha uwezo wa wazawa.

**Jukumu la USAID:**
USAID lazima pia ielewe jukumu letu la kipekee ndani ya mfumo. Uwezo wetu mkubwa kama mfadhili utatofautiana kulingana na uwezo uliopo, mahusiano, na rasilimali za na zilizo miongoni mwa wadau kutoka katika sekta mbalimbali, mashirika ya kimataifa na wafadhili ndani ya mfumo wa kizawa. Jukumu hili mara nyingi litakuwa zaidi ya mbinu za kawaida za mipango ya maendeleo na usaidizi wa kibinadamu. Inaweza kuwa uwezo wetu wa kuunganisha wadau kutoka katika sekta mbalimbali na vyanzo vinavyohitajika vya usaidizi wa kiufundi, kuleta pamoja wadau kutoka katika sekta mbalimbali na wahusika wa kimataifa, kuimarisha mahusiano na miunganisho katika mfumo mzima, au kuelekeza rasilimali kwa wahusika wakuu wazawa ili kuimarisha ushawishi wao. Kuwa na uelewa kamili wa jukumu la kipekee tunalotekeleza katika mfumo wa kizawa pia kutaelekeza mbinu tutakayotumia.

Kama sehemu ya uzingatiaji huu, lazima tuzingatie jukumu ambalo rasilimali zetu za kifedha hutekeleza katika

### TAARIFA KUHUSU RUZUKU KWA WADAU KUTOKA KATIKA SEKTA MBALIMBALI NA HATARI

Kama inavyooneshwa kote katika Kanuni za Mipango ya Ufanisi ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa, uamuzi wa kutoa ruzuku kwa mhusika mzawa kwa madhumuni ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa lazima utokane na uzingatiaji wa masuala ya mipango na wala si masharti ya ununuzi na usaidizi. Uamuzi huo unapaswa kuibuka kutokana na uchanganuzi wa kina wa mfumo wa kizawa na kuzingatia makusudi aina za uwezo na mbinu zinazohitajika ili kuboresha utendaji wa muda mfupi na muda mrefu wa wahusika na mifumo ya kizawa ili kukuza umiliki wa ndani na kuendeleza matokeo ya maendeleo. Kuweka msingi wa uamuzi huu katika uzingatiaji wa masuala ya mipango kunaweza kuhakikisha kwamba ruzuku inakidhi mahitaji ya Mshirika Mzawa na jamii na kwamba hatari yoyote inayohusishwa na ruzuku kwa mhusika wa mzawa inatathminiwa katika muktadha wa mahitaji ya jumla ya mipango na manufaa yanayoweza kupatikana.

Zaidi ya hayo, kutathmini hatari kwa USAID na kutathmini uwezo na mahitaji ya wenyeji si jambo sawa. Yote mawili hutekeleza jukumu muhimu, lakini haifai kubadilisha tathmini ya hatari kwa tathmini ya uwezo wa kizawa wala kubadilisha mpango wa udhibiti wa hatari kwa mpango wa kuimarisha uwezo. Ili kuongeza ufanisi, kuhakikisha ufanisi na kuwezesha uwajibikaji wa pande zote, tathmini ya hatari na mipango ya kupunguza athari hasi inapaswa kufanywa kandokando na tathmini za Kuimarisha Uwezo wa Wazawa na mipango ya utekelezaji, lakini yote yanapaswa kufanywa moja baada ya lingine na kwa ushirikiano na wadau kutoka katika sekta mbalimbali.

Tathmini ya jumla ya fursa na matishio inalingana na mwongozo wa USAID kuhusu udhibiti wa hatari kwa biashara, Tamko la Shirika la Hatari Zinazoweza Kuvumilika na Mkakati wa Ununuzi na Usaidizi. Kwa kufanya hivi, USAID inaweza kujikita katika matokeo chanya ya mipango inayohusishwa na kushirikiana na washirika wazawa na kuwa na ujasiri kwamba uamuzi wetu wa kutoa ruzuku kwa mhusika mzawa utapelekea ruzuku inayoweza kusimamiwa ipasavyo kifedha na kusalia kuwa muhimu katika kuchangia mafanikio na uendelevu wa usaidizi wa kibinadamu na matokeo ya maendeleo.

kuendeleza Kuimarisha Uwezo wa Wazawa. Rasilimali zetu zinaweza kuwa njia kuu ya kuwezesha—kwa njia isiyo ya moja kwa moja na ya moja kwa moja—uimarishaji wa uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali. Rasilimali zinazotolewa kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa wadau kutoka katika sekta mbalimbali kupitia washirika wa kimataifa zinaweza kuwasaidia wadau kutoka katika sekta mbalimbali kupata ustadi maalum na kuunda miunganisho mipya ya mtandao. Zaidi ya hayo, kuwafadhili wadau kutoka katika sekta mbalimbali kupitia ruzuku za moja kwa moja kunaweza kuimarisha uwezo wao wa kujifunza kwa kufanya na kuimarisha uongozi na ushawishi wa kizawa, ambapo kimtawalia ni mbinu muhimu na aina ya uwezo. Hatimaye, uamuzi wa kuwezesha Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kupitia ruzuku isiyo ya moja kwa moja au ya moja kwa moja kwa wadau kutoka katika sekta mbalimbali unapaswa kufanywa kulingana na uelewa wa kina wa kwa nini mbinu iliyochaguliwa inafaa zaidi kuwezesha uwekezaji katika uwezo wa kizawa kuchangia katika mabadiliko mapana ya mifumo na matokeo endelevu. Hapo tunaweza kuwa na imani kwamba ruzuku itakuwa zaidi ya muamala wa kifedha tu.

## 3 Kanuni ya 3: Panga na upime maboresho ya utendaji ukishirikiana na washirika wazawa.

Uwezo ni aina ya uwezekano na hauonekani hadi unapotumika. Hivyo, uzingatiaji wowote wa mipango kuhusu Kuimarisha Uwezo wa Wazawa lazima upange na kupima utendaji ulioboreshwa—sio uwezo fiche. Ni kupitia utendaji, au kutumia uwezo, ambapo wadau kutoka katika sekta mbalimbali huonesha mafanikio ya vipaumbele vyao wenyewe vya maendeleo. Hii inamaanisha kwamba nadharia za mabadiliko na mipango ya ufuatiliaji, kutathmini na kujifunza kutoka kwa uwekezaji wa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa lazima ijikite katika mabadiliko yanayoweza kuonekana katika utendaji wa wahusika na mifumo, sio tu vipengele vinavyoweza kuhesabika kwa urahisi kama vile idadi ya mafunzo yaliyohudhuriwa au mipango au taratibu iliyobuniwa. Zaidi ya hayo, USAID na washirika wa kimataifa lazima watoe kipaumbele kwa kushirikisha washirika wazawa—kupitia mahusiano ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja ya ruzuku—ili kubainisha vipaumbele vya kuboresha utendaji na kuongoza kwa pamoja utambuzi wa vipimo vya utendaji na kubuni mipango ya kupima.

> **Utendaji** unarejelea kiwango ambacho mhusika anaweza kufikia matokeo yake yaliyokusudiwa kwa ufanisi na uthabiti. Ni jambo muhimu la kuzingatia katika kubainisha iwapo uwezo umebadilishwa.
>
> **Uboreshaji wa Utendaji** ni mbinu ya mipango inayorejelea mchakato wa makusudi unaofanywa ili kuboresha uwezo wa mhusika kutimiza malengo yake.

Kufuatilia utendaji kwa ufanisi kunahitaji kuchagua mbinu ya kupima inayofaa. Kwa sababu mahitaji ya kuripoti yanaweza kuwasilisha vichocheo vya kupotosha ambavyo vinaweza kupelekea kuzingatia matokeo ya muda mfupi badala ya matokeo ya maendeleo endelevu, marudio na msisitizo wa kuripoti unapaswa kulenga makusudi kufuatilia maendeleo yanayoongezeka mintarafu ya mabadiliko ya muda mrefu. Kujumuisha viashirio vya matokeo katika mpango wa ufuatiliaji husaidia katika kufuatilia maendeleo dhidi ya vipindi vya wakati na bajeti zilizopangwa lakini havipaswi kutumiwa kama mbadala wa vipimo halisi vya kiwango cha matokeo vya uboreshaji wa utendaji. Zaidi ya hayo, wakati wowote inapowezekana, vipimo na mbinu za utendaji ambazo tayari zinatumiwa na shirika la kizawa, ikiwa ni pamoja na zilizowekwa chini ya mamlaka za kizawa au viwango vingine vya kizawa, vinapaswa kutumika badala ya vilivyoundwa kwa madhumuni pekee ya kuripoti kwa USAID.

Ufuatiliaji wenye ufanisi wa utendaji pia unahitaji kubainisha ni zana zipi zinafaa zaidi kwa madhumuni yapi—kipimo cha utendaji, kupanga utekelezaji wa uwezo au kupunguza hatari:

**Zana za Kupima Utendaji** hufuatilia na kupima kiwango cha kuboreka kwa utendaji kama matokeo ya usaidizi wa kuimarisha uwezo. Husaidia USAID, washirika wake na jamii za kizawa kugundua iwapo wadau kutoka katika sekta mbalimbali wanaweza kutumia vyema zaidi uwezo wao kutekeleza majukumu ndani ya mifumo yao ya kizawa kutokana na usaidizi wetu. Zana hizi, hata hivyo, lazima zitofautishwe na zana za kuchochea mchakato wa uimarishaji wa uwezo na zile za kutambua na kudhibiti hatari.

**Zana za Kupanga Utekelezaji wa Uwezo** huwezesha mchakato unaotumiwa na wadau kutoka katika sekta mbalimbali kutambua vipaumbele vyao wenyewe vya kuboresha utendaji na kupata motisha ya kumiliki na kusimamia maendeleo yao wenyewe. Zana hizi pia zinaweza kusaidia USAID na washirika wa kimataifa kupata habari kuhusu uwezo wa kizawa uliopo na aina ya usaidizi wa kuimarisha uwezo ambao wadau kutoka katika sekta mbalimbali wanatamani na kuhitaji.

**Zana za Kupunguza Hatari** zinakusudiwa kimsingi kutathmini na kusaidia kubuni mipango ya kupunguza hatari kwa USAID kwa kushirikiana na shirika lolote. Ingawa zana hizi zinaweza kutambua uwezo uliopo na maeneo ya kuboresha ndani ya mashirika ya ndani, hazipaswi kutumiwa kama mbadala wa kuchochea mchakato wa kuimarisha uwezo wa kizawa au kupima kuboreka kwa utendaji kama matokeo ya usaidizi wa kuimarisha uwezo.

Ingawa kila moja kati ya zana hizi ni muhimu kwa sababu tofauti, USAID na washirika wake wanapaswa kukumbuka kwamba wadau kutoka katika sekta mbalimbali mara nyingi huombwa au kuhitajika kushiriki katika tathmini zinazofanywa na wafadhili mbalimbali, washirika wa kimataifa na aina nyingine za mashirika, kama vile mashirika ya serikali ambayo hutoa usajili na watoa huduma wengine ambao hutoa vibali au vyeti rasmi. Kutokana na hilo, wadau kutoka katika sekta mbalimbali mara nyingi hukabiliwa na "kuchoshwa na tathmini nyingi." Hata hivyo, kutokana na ukosefu uliopo wa usawa katika mamlaka, wadau kutoka katika sekta mbalimbali huenda wasiwe na ujasiri wa kueleza wasiwasi wao au kukataa maombi au mialiko ya kushiriki katika tathmini za ziada za utendaji. Hivyo, kabla ya kufanya tathmini yoyote mpya na mhusika mzawa, USAID lazima kwanza iombe na kutumia matokeo ya tathmini nyingine za hivi karibuni zinavyofaa. Aidha, Shirika lazima lishiriki matokeo ya tathmini yoyote iliyoendeshwa na USAID iliyofanywa na wadau kutoka katika sekta mbalimbali katika muundo unaoweza kufikiwa na kujadili matokeo haya na wadau kutoka katika sekta mbalimbali waliohusika katika tathmini. Kushiriki matokeo yanayoweza kufikiwa na kuyaelewa kwa pamoja na wadau kutoka katika sekta mbalimbali hutoa fursa ya kujifunza inayoheshimu ahadi yetu ya ushirikiano wenye usawa.

Hatimaye, upimaji wa utendaji wa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa lazima uunganishwe na mabadiliko ya kimfumo ambayo USAID na wadau kutoka katika sekta mbalimbali wanataka. Kuanzia uchanganuzi wetu wa mifumo hadi uamuzi wetu wa kimkakati na makusudi wa kuwekeza katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kama mbinu, kipaumbele cha kimkakati cha USAID ni kuboresha uwezo wa mifumo ya kizawa ili kuzalisha na kudumisha matokeo ya maendeleo kwa kushirikiana na wadau kutoka katika sekta mbalimbali. Kupanga na kupima utendaji kunaweza kuisaidia USAID na washirika wetu kuelewa mahusiano kati ya mchakato wa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa na utendaji ulioboreshwa wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali, na pia kati ya utendaji ulioboreshwa wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali na matokeo ya maendeleo katika ngazi ya mfumo baada ya muda. Kulenga upimaji wa utendaji pamoja na nadharia hii ya mabadiliko kunaweza kuwezesha kujifunza kunakotokana na ushahidi na kufanya maamuzi muhimu ya kurekebisha na kuboresha mipango ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa. Zaidi ya hayo, maarifa haya huipatia USAID ujasiri wa kusema kwa dhati jinsi uwekezaji wetu katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa unavyochangia katika matokeo ya maendeleo endelevu katika sekta zote na kuhalalisha jukumu la USAID katika kukuza umiliki wa kizawa, uendelevu na maadili ya kidemokrasia kila mahali.




Picha kwa Hisani ya: Jamie Barnett/FHI 360



# III. KANUNI ZA UBIA WENYE USAWA KATIKA KUIMARISHA UWEZO WA WAZAWA

> "USAID lazima ibadilishe muundo wetu kutoka kushirikiana **kwa ajili ya** hadi kushirikiana **pamoja na.**"

Ukosefu wa usawa wa mamlaka mara nyingi ndiyo kiini cha changamoto za maendeleo za kimataifa. Mamlaka yanaweza kuoneshwa kwa njia nyingi. Yanaweza kuoneshwa kwa kulazimisha, kama "kuwatawala" wengine. Yanaweza kuoneshwa ili kutafuta mtazamo wa pamoja na kuunda ushirikiano unaoendeleza matokeo ya pamoja, kama "kushiriki mamlaka" na wengine. Yanaweza kutumiwa na kila mtu, kama "uwezo wa" kuunda maisha yake na ulimwengu unaomzunguka. Na yanaweza hata kuoneshwa kupitia uwezo wetu wa kufikiria na kutumaini kwa kupata na kutumia "uwezo ulio ndani yetu" wenyewe.[2]

Kutokana na hilo, USAID inatambua uwezo wa asili unaomilikiwa na wafadhili rasmi wa usaidizi wa maendeleo na imejitolea kwa kanuni nne za ubia wenye usawa katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa ambazo zimefafanuliwa katika sehemu hii. Kanuni hizi zitawezesha mipango ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa katika sekta na kanda mbalimbali na kuongoza ushirikiano unaolingana na vipaumbele vya ndani; kutumia mbinu inayolingana na uwezo au rasilimali; kuzingatia na kupunguza matokeo yasiyotarajiwa; na unaotokana na kuheshimiana na kutendeana.

Kwa kutumia uwezo wetu kujitolea kwa kanuni zifuatazo, pamoja na kanuni za mipango yenye ufanisi ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa ilivyoelezwa katika sehemu iliyotangulia, USAID inalenga kuhamisha mamlaka kwa wadau kutoka katika sekta mbalimbali ili kusaidia jamii imara na thabiti zaidi zinazoweza kujumuisha maoni na asili anuwai zaidi. Kuimarisha Uwezo wa Wazawa unaojumuisha watu ambao huenda vinginevyo wakakabiliwa na ubaguzi na kutengwa kisheria, kijamii na kiuchumi unaweza kubadilisha uwezo wa mtu binafsi wa kufanya jambo na kuunda fursa za ushirikiano mpya na tofauti miongoni mwa watu, mashirika

2 Gaventa, John. "Finding the spaces for change (Kutafuta nafasi za mabadiliko): A power analysis (Uchanganuzi wa mamlaka)." IDS Taarifa ya 37, namba 6, (Novemba 2006): 23–33. https://doi.org/10.1111/j.1759-5436.2006.tb00320.x.

Picha kwa Hisani ya: Neil Brandvold kwa ajili ya USAID

na mitandao. Kujumuisha watu makusudi kiasili huleta mitazamo na rasilimali mpya ili kupanua uwezo wa uzalishaji wa kazi yetu na hubadilisha majukumu ya wadau kutoka katika sekta mbalimbali wanaoweza kuleta mabadiliko chanya kwa ajili ya maendeleo endelevu.

## 4 Kanuni ya 4: Jumuisha uimarishaji wa uwezo na vipaumbele vya wazawa.

USAID imejitolea kusaidia nchi washirika kufikia malengo yao wenyewe ya kibinadamu na maendeleo, huku pia ikitumia uwekezaji wa walipakodi wa Marekani kutoa matokeo ya muda mrefu zaidi ya maendeleo endelevu. Hata hivyo, vipindi vifupi vya mizunguko ya bajeti na kuepuka hatari wakati mwingine kunaweza kupotosha Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kuelekea kwa kukuza ujuzi kwa manufaa ya muda mfupi, kama vile usimamizi wa kifedha ambao ni mahususi kwa mfadhili au uwekaji chapa na alama. Ingawa utekelezaji wa usaidizi rasmi wa maendeleo mara nyingi uhitaji shughuli za kupunguza hatari, ambazo ni muhimu katika kazi yetu na usimamizi wa rasilimali, usaidizi wa kukuza ujuzi huu haupaswi kufasiriwa kama Kuimarisha Uwezo wa Wazawa ambao huendesha mabadiliko ya kijamii ya muda mrefu. Hata hivyo, kutilia mkazo kupita kiasi katika kufuata sheria au uwezo wa kutoa matokeo ya muda mfupi kunaweza kuwa na athari potofu zinazoweza kuongeza utegemezi kwa wafadhili wa kimataifa na kudhoofisha uwezo wa kukabiliana na changamoto kwa kukandamiza uzalishaji wa mapato ya wazawa. Baada ya muda, usaidizi huo unaweza kudhoofisha wito wa mashirika ya kizawa.

Hivyo, pindi uamuzi wa kuwekeza katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa unapofanywa, lazima tuelekeze umakini wetu katika kuwashirikisha wadau kutoka katika sekta mbalimbali ili kutambua vipaumbele vya kuimarisha uwezo pamoja na kuwezesha uboreshaji wa utendaji katika maeneo hayo, bila kujali iwapo tutaingia katika uhusiano wa ufadhili na wahusika hao. Ili kutafuta ubia wenye usawa wa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa, USAID itafuata mwelekeo wa "usifanye jambo lolote linalotuhusu bila kutujumuisha"—kauli mbiu iliyoanzishwa katika vuguvugu za kisiasa huko Ulaya Mashariki na kufanywa kuwa maarufu na vuguvugu ya haki za walemavu.[3] Hii inamaanisha kwamba hakuna maamuzi ya mipango kuhusu Kuimarisha Uwezo wa Wazawa yanapaswa kufanywa bila ushiriki halisi wa wanachama wa kikundi kinachoathiriwa na mpango huo. USAID lazima ibadilishe muundo wetu kutoka kushirikiana "kwa ajili ya" hadi kushirikiana "pamoja na."

USAID inapotambua mamlaka ya asili miongoni mwa wadau kutoka katika sekta mbalimbali na jamii za kizawa, tunaunga mkono, badala ya kudhoofisha, uwezo wa kufanya mambo wa wenyeji na maendeleo yanayoongozwa na wenyeji. Maamuzi kuhusu ni uwezo gani wa kuimarisha, mbinu zipi zinaweza kuwa na ufanisi zaidi, na ni malengo yapi ya uboreshaji wa utendaji ya kuweka lazima yajikite katika matamanio na malengo ya wadau kutoka katika sekta mbalimbali. Vile vile, USAID inapotambua ukosefu wa usawa au kutengwa kwa vikundi fulani vya wadau kutoka katika sekta mbalimbali, tunaweza kutumia uwezo wetu makusudi kuwajumuisha, kuwainua na kuwawezesha, badala ya kuendeleza kutengwa kwao. Zaidi ya hayo, vipaumbele vya watu vinaweza kuwa tofauti na vipaumbele vya mashirika ambayo huchukua hatua kwa niaba yao, kwa hivyo USAID inapaswa kutafuta fursa za kusikiliza moja kwa moja kutoka kwa watu badala ya wawakilishi ambao wanaweza kuchukua au kutochukua hatua kwa niaba yao. USAID lazima pia itambue kwamba hali na mahitaji ya wazawa yanaweza kubadilika au kugeuka, hivyo Kuimarisha Uwezo wa Wazawa unapaswa kudhibitiwa ipasavyo kulingana na hali husika ili kushughulikia mabadiliko yasiyotabirika na mahitaji yanayojitokeza ya wadau kutoka katika sekta mbalimbali.

Hatimaye, wadau kutoka katika sekta mbalimbali wanapotambua vipaumbele, na pia kuthamini na kumiliki mchakato wa mabadiliko, wana uwezekano mkubwa zaidi

---

3 Charlton, James I. Nothing About Us Without Us (Usifanye Jambo Lolote Kutuhusu Bila Kutujumuisha): Disability, Oppression and Empowerment (Ulemavu, Ukandamizaji na Uwezeshaji). (1998) Berkeley, CA: University of California Press.

Smorgorzewski, Kazimierz, "Poland's Foreign Relations (Mahusiano ya Kigeni ya Poland)." katika Slavonic and East European Review (Uhakiki wa Slavonia na Ulaya Mashariki) (1938), iliyonukuliwa katika Janine Owens, "Exploring the Critiques of the Social Model of Disability (Kuchunguza Uhakiki wa Muundo wa Kijamii wa Ulemavu): The Transformative Possibility of Arendt's Notion of Power (Uwezo wa Kuleta Mabadiliko wa Dhana ya Arendt ya Mamlaka)." katika Sociology of Health and Illness (Sosholojia ya Afya na Magonjwa) (Desemba 2014).

wa kufaulu katika kufikia na kudumisha mabadiliko chanya muda unavyosonga. Hivyo, kwa kushughulikia vipaumbele vya wazawa, USAID inaweza kupata ujasiri zaidi kwamba uwekezaji wake katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa utaleta maendeleo endelevu.

## 5 Kanuni ya 5: Tambua vyema na kutumia uwezo uliopo.

Wadau kutoka katika sekta mbalimbali kwa muda mrefu wameelezea matatizo yao kuhusu jinsi wafadhili wa kimataifa na mashirika mengine ya kimataifa yanavyowaelewa na kuwasaidia. Tena na tena wanaangazia uwezo mkubwa wa ndani ambao tayari upo katika jamii zao na ambao mara nyingi hupuuzwa na wahusika wa kimataifa. Hivyo, USAID inapotoa usaidizi ili kuimarisha uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali, tutatumia mbinu inayojikita kwa uwezo au rasilimali ambayo husaidia jamii za kizawa kutambua uwezo wao na kufikiria njia ambazo wanaweza kutumia rasilimali hizo kukidhi mahitaji ya jamii zao. Utendaji unaolingana na uwezo kimsingi hupinga mbinu za kawaida za mahusiano ya mamlaka kati ya watu, miongoni mwa mashirika na ndani ya jamii. Badala ya kutenda kwa kutumia nafasi ya kuwa na mamlaka juu ya mwingine, mbinu zinazolingana na uwezo au rasilimali hufungua njia ya kupata ubia wenye usawa kwa kuhitaji uakisi wa kina wa mienendo ya mamlaka katika mahusiano yetu na kulenga kushiriki mamlaka na kutoa uwezo, pamoja na kuimarisha uwezo wa wazawa.[4]

USAID na washirika wake hawatalenga kutambua mapungufu au udhaifu. Badala yake tutatumia mbinu za kushiriki zinazothamini uwezo uliopo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali na uwezo wa mifumo ya kizawa, ikiwa ni pamoja na maarifa, desturi na imani asili za kizawa. Kwa kuandamana na jamii za kizawa kutambua

4 Mathie, Alison, Cameron, Jenny, na Gibson, Katherine. "Asset-based and citizen-led development (Maendeleo yanayolingana na rasilimali na yanayoongozwa na raia): Using a diffracted power lens to analyze the possibilities and challenges (Kutumia lenzi finyu za mamlaka kuchanganua uwezekano na changamoto) ," Progress in Development Studies (Maendeleo Katika Utafiti wa Maendeleo), 17, namba 1 (Februari 2017): 1–13, https://doi.org/10.1177/1464993416674302.

Stuart, Grame. "Strengths-based practice and ABCD (Utendaji unaolingana na uwezo na ABCD)." https://sustainingcommunity.wordpress.com/resources-for-students/strengths-based-approaches/

### KUANGAZIA MBINU YA KUIMARISHA UWEZO WA WAZAWA: MAENDELEO CHANYA YA VIJANA

Kushirikisha kwa pamoja maoni na ujuzi wa vijana bilioni 2.4, wanaofafanuliwa na USAID kama watu wenye umri wa kati ya miaka 10 na 29, ni muhimu katika kufikia maendeleo endelevu. Zana moja ya mpango inayoakisi jinsi mbinu inayolingana na uwezo inaweza kutumika kuwezesha Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kwa pamoja ni Mfumo wa Maendeleo Chanya ya Vijana (PYD). PYD ni mbinu ya makusudi inayothamini umuhimu wa mahusiano ya kijamii ambayo huwashirikisha vijana ndani ya jamii zao kwa njia inayotambua na kuimarisha uwezo wa vijana ili kukuza matokeo chanya. Badala ya kuwaona vijana kama wapokeaji wa usaidizi wa kimyakimya, mbinu ya PYD inaweza kuhakikisha kwamba vijana wanatambuliwa kama mawakala wa maendeleo yao wenyewe na kwamba Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kwa vijana unawasaidia kutumia uwezo wao kuunda maisha yao na jamii inayowazunguka. Mbinu ya PYD huwahusisha vijana katika kuunda na kusanifu mipango pamoja na kufanya maamuzi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Kuimarisha Uwezo wa Wazawa ambazo:

- Hutambua na kutumia rasilimali za vijana kama vile ujuzi muhimu wa kijamii au ujuzi wa kitaaluma au kiufundi na maarifa.
- Hukuza uwezo wa vijana wa kufanya mambo kwa kuwasaidia kuweka malengo, kubuni utambulisho wao wenyewe na kupata ujasiri kwamba wanaweza kutimiza malengo hayo.
- Huunganisha vijana na mazingira ya usaidizi kupitia ukufunzi na upatikanaji wa washauri.

NYENZO: [Positive Youth Development Measurement Toolkit (Seti ya Zana za Kupima Maendeleo Chanya ya Vijana)]

na kutumia uwezo na rasilimali zilizopo, lakini pengine zisizotambuliwa au zisizothaminiwa vya kutosha, USAID inaweza kusaidia mashirika na watu kutambua wenyewe vikwazo vinavyowakabili, kutambua rasilimali na uwezo ambao tayari wanao wa kushughulikia vikwazo hivi, na kuthamini uwezo wao wenyewe wa kufanya marekebisho yanayohitajika katika hali husika. Mchakato huu utawasaidia wadau kutoka katika sekta mbalimbali kuongoza juhudi za kuweka ajenda zao wenyewe, kubuni masuluhisho, na kutoa uwezo, uongozi, na rasilimali zao ili kufanya masuluhisho hayo kutimia. Kwa kutumia uwezo na rasilimali zilizopo, usaidizi wetu utachangia katika matokeo ya maendeleo endelevu zaidi.

Kuzingatia inavyofaa uwezo na rasilimali ni zaidi ya kutambua tu kwamba kila mhusika mzawa ana uwezo wake mwenyewe uliopo, hata hivyo. Inamaanisha kwamba asili halisi ya mbinu ya kukuza uwezo inafaa katika kuboresha ufanisi wa kila mhusika katika mfumo wake wa kizawa. Ili kufikia lengo hili, hatutaingia katika ushirikiano tukiwa na maono yaliyowekwa mapema ya jinsi "hali ya mwisho" ya wadau kutoka katika sekta mbalimbali itafikiwa wala kutumia mbinu ya kawaida ya pamoja kuwezesha Kuimarisha Uwezo wa Wazawa. Kuangazia Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kwa kutumia dhana iliyobuniwa mapema kuhusu jinsi mhusika "mzuri" au "mwenye uwezo" anavyoonekana kunaweza kudhoofisha mchakato wa ushirikishaji na ufanisi wa mipango. Ingawa utendaji unaweza kupimika dhidi ya matokeo ya kawaida, uwezo unaweza kuwa wa aina anuwai zinazowezesha mafanikio ya utendaji. Uzoefu mwingine, mitindo na ulinganisho wa kimataifa unaweza kutoa taarifa za kuelewesha lakini haupaswi kamwe kutumiwa kufanya maamuzi. Tunapaswa kutarajia kila mhusika mzawa kukua kwa njia tofauti. Lazima tutoe usaidizi wa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kwa kila mhusika mzawa kulingana na mazingira na vipaumbele vya kipekee, uwezo, fursa na stahamala dhidi ya hatari. Kwa sababu hii, lazima tuache jukumu la kuelekeza na kuchukua jukumu la kuwezesha katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa—jukumu ambalo huwatia msukumo na kuwatia moyo wadau kutoka katika sekta mbalimbali kutambua "uwezo walio nao" na kutimiza uwezo wao wa binafsi.

## 6 Kanuni ya 6: Zingatia na kupunguza athari zisizokusudiwa za uwezeshaji wetu wa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa.

Kama uingiliaji kati mwingine wa maendeleo, mbinu za kuimarisha uwezo yamkini zinaweza pia kusababisha madhara yasiyotarajiwa. Kwa sababu ni maingiliano machache ya kijamii hukosa kupendelea upande wowote kimamlaka, mamlaka na siasa ni muhimu sana katika matokeo ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa. Kabla ya kujihusisha na wadau kutoka katika sekta mbalimbali, USAID inapaswa kutafakari kuhusu miundo ya mamlaka inayoonekana, iliyofichwa na isiyoonekana katika mfumo wa kizawa na jinsi ambavyo inaweza kudhihirika miongoni mwa wahusika katika mfumo wa kizawa na katika maingiliano yetu na washirika wazawa. Kuzingatia jinsi mamlaka huathiri ufanyaji maamuzi na mazingira ya kisiasa au kuweka ajenda kunaweza kutusaidia kubuni ushirikiano unaotokana na kuheshimiana na kuaminiana na kusaidia kusawazisha tofauti za mamlaka kupitia mipango ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa.

Mifumo ya kizawa inaweza kuwa na sifa ya mipangilio madhubuti ya kujumuisha na kutenga watu ambayo huakisi ushindani kwa ajili ya rasilimali na mamlaka kupitia majukumu rasmi na yasiyo rasmi, historia, mahusiano, imani za kitamaduni na kaida nyingine za kijamii. Kufikia na kudumisha uwezo wa wazawa ulioimarishwa na mabadiliko chanya ya mifumo ya kizawa kunahitaji kushughulikia motisha na mienendo ya mamlaka miongoni mwa wadau kutoka katika sekta mbalimbali katika mfumo wa kizawa. Hata hivyo, baadhi ya shughuli za kuimarisha uwezo zinaweza kuathiri majukumu, ushindani na maslahi yaliyowekwa kwa namna ambayo huhamisha mamlaka na ushawishi kutoka kwa watu na vikundi fulani hadi kwa wengine. Ingawa mabadiliko haya mara nyingi yanaweza kuwezesha mabadiliko chanya na maendeleo endelevu katika ngazi ya mifumo, yanaweza pia kuunda au kuzidisha ushindani au mgogoro. Kwa hivyo, USAID lazima itathmini uwezekano wa madhara kwa kutumia mbinu zinazozingatia migogoro, uchumi wa kisiasa na "zisizodhuru". Mbinu hizi zinaweza kusaidia kutambua mienendo iliyopo ambayo vinginevyo



Picha kwa Hisani ya: Bobby Neptune kwa ajili ya USAID

inaweza kusababisha mgogoro au matokeo mengine yasiyotarajiwa, na lazima tutumie matokeo hayo kupunguza athari zozote hasi zinazoweza kutokea.

Katika hali fulani, hii inaweza kuhitaji kuwezesha na kuinua maoni ya watu waliotengwa na walio na uwakilishi mdogo hadi hadhi yenye usawa bila kuwaweka hatarini. Vikundi hivyo vitatofautiana kulingana na mfumo wa kizawa na vinaweza kujumuisha lakini sio tu, wanawake na wasichana, watu wenye ulemavu, mashoga, wakimbizi, wahamiaji, Wenyeji, vijana, wazee, vikundi vya kidini vya watu wachache, vikundi vya rangi na makabila ya watu wachache, watu wa matabaka ya chini na watu wenye mahitaji ya afya ya akili. Kila mtu na jamii yenye utambulisho na uzoefu mbalimbali, ni muhimu katika mabadiliko ya jamii zao. Kujumuishwa kwao kwa usawa katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa husaidia kupunguza uwezekano wa matokeo yasiyotarajiwa kwa kuthibitisha na kuboresha uelewa wetu wa maarifa ya mazingira, kuimarisha kuaminika kwa uingiliaji kati wa mipango inayofadhiliwa na USAID, kuongeza uwezekano wa masuluhisho yanayopendekezwa kukubaliwa na kudumishwa na kuimarisha uwezo wa USAID wa kushughulikia changamoto za kibinadamu na maendeleo kwa ukamilifu.

Katika hali nyingine, kufikia maono ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa yaliyoelezwa katika sera hii kutahitaji USAID na washirika wake kuchunguza upya majukumu yetu katika maendeleo na kuchunguza mapendeleo na dhana zetu kabla ya kuwashirikisha wadau kutoka katika sekta mbalimbali. Urithi wa kihistoria wa ukoloni na kutengwa kwa watu umezalisha ukosefu wa usawa katika mamlaka ambao una athari zinazoendelea kwenye mipango ya kibinadamu na maendeleo, na wahusika mbalimbali huona na kuathiriwa na athari hizo kwa njia tofauti. USAID lazima ikubali wakati michakato yetu wenyewe inaweza kukuza ukosefu huu wa usawa bila kukusudia, kwa sababu ukosefu huu wa usawa huhatarisha matokeo na uendelevu wa mipango ya usaidizi wa kigeni ya USAID. Urithi huu wa kihistoria unachochewa zaidi na vikwazo vya rasilimali, ambapo washirika wazawa mara nyingi hujitahidi kupata au kudumisha ufadhili kwa kufungamanisha shughuli zao na vipaumbele vya wafadhili wa kimataifa, hivyo kuwahitaji wadau kutoka katika sekta mbalimbali kutenga muda na rasilimali nyingi kwa jitihada hizo. Zaidi ya hayo, vipaumbele vya sera ya USAID na wafadhili wengine wa kimataifa vinaweza kubadilika ghafla, jambo linaloweza kusababisha mabadiliko ya ufadhili kwa kuelekezwa kwa vipaumbele vipya na tofauti. Kutokana na hilo, harakati za wadau kutoka katika sekta mbalimbali za

kutafuta ufadhili wa wafadhili wa kimataifa, hasa ikiwa hazina mwendelezo, zinaweza kuvuruga sana mifumo ya kizawa na zinaweza kudhoofisha uaminifu wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali na wenzao. Hivyo, shughuli zinazokusudiwa kuendeleza vipaumbele vya wafadhili, badala ya kuimarisha uwezo wa washirika wazawa kutekeleza majukumu mapya au yaliyopo kwa ufanisi zaidi ndani ya mfumo wa kizawa, huleta hatari na madhara yanayoweza kutokea kwa washirika wazawa. Hatimaye, USAID lazima ichukue tahadhari ili kupunguza madhara yanayoweza kutokana na wenyeji kukubali vipaumbele vya wafadhili wa kimataifa na kudhoofisha uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali kufanya kazi ili kutimiza matamanio na malengo yao wenyewe au dhamira za shirika.

## 7 Kanuni ya 7: Dumisha ushirikiano na washirika wazawa.

Uimarishaji wenye mafanikio wa uwezo wazawa kiasili unahusisha kushirikiana kutambua malengo, kuimarisha uwezo na kupima mabadiliko muda unavyosonga. Ili kuwezesha ushirikiano chanya na kutoka kwake kupata uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa, USAID na washirika wake wanapaswa kuangazia Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kwa msingi wa kuheshimiana na kuaminiana. Hii inamaanisha USAID na washirika wake wanatambua na kuthamini matamanio na malengo, uwezo na rasilimali tofauti ambazo kila mmoja huleta kwenye ushirikiano. Ili kufanya hivi, USAID inapaswa kueleza wazi kwanini tuliamua kuwekeza katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa na mabadiliko tunayotumai yatapatikana kutoka kwake, huku pia tukikubali ukweli kwamba wadau kutoka katika sekta mbalimbali wanaweza kuwa na sababu tofauti lakini ambazo ni halali pia za kutafuta usaidizi wa kuimarisha uwezo. Pia tunapaswa kujumuisha muda na rasilimali za kutosha katika muundo wa mpango ili kuweka mazingira wezeshi ya kuunda masuluhisho ya maendeleo pamoja, kwa kuwa hili linaweza kusaidia kukuza kuheshimiana na kuaminiana.

**Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kunahitaji kumilikiwa na wenyeji. Mapatano katika ushirikiano yanaweza kusaidia kupelekea umiliki huo wa wenyeji.**

**Mapatano** ni hali chanya au mtazamo wa pamoja kuhusu uhusiano ambapo washirika wawili (au wengi) hulenga kusawazisha tofauti za kimamlaka kwa kujitahidi kupata ubia wa kukubaliana unaoleta manufaa kwa kila mshirika kupitia mahusiano yanayotokana na uaminifu na heshima. Hii hupatikana USAID na mshirika(washirika) wake wanaposhiriki au kubadilishana taarifa na kuchukua hatua mintarafu ya malengo ya pamoja, kama vile kupitia uwajibikaji wa pande zote, ambao ni mchakato ambao kupitia kwake washirika hukubali kuwajibika kwa ahadi ambazo wameahidiana kwa hiari.

Kwa kufanya mapatano[5], USAID na washirika wazawa pia wanapaswa kuhakikisha kila mmoja wao anawajibika katika mipango ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa. Uwajibikaji wa pande zote ni mchakato ambapo washirika wawili au zaidi hukubali kuwajibika kwa ahadi wanazoahidiana kwa hiari. Hutegemea maafikiano kuhusu ajenda za pamoja na kutoa kipaumbele kwa utendaji wenye mafanikio wa ushirikiano. Uwajibikaji wa pande zote unaweza kutekelezwa kwa njia nyingi na miongoni mwa wahusika wengi, kama vile miongoni mwa wafadhili na viongozi wa kizawa, mashirika ya kizawa na tanzu zao, mitandao na wanachama wao, na wananchi na serikali zao au watoa huduma. Ushirikiano wa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa unaojitolea kwa kuwajibika kwa pande zote unaweza kukuza ushirikishaji wenye uwazi na usawa ambao huleta matokeo yanayothaminiwa na pande zote.

Uwajibikaji wa pande zote pia hutoa fursa kwa USAID kujifunza kutoka kwa wadau kutoka katika sekta mbalimbali wakati wote wa kubuni na kutekeleza shughuli za Kuimarisha Uwezo wa Wazawa. Njia moja ambayo USAID inaweza kutekeleza ahadi yetu ya kuunga mkono uwajibikaji wa pande zote katika mipango ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa ni kwa kukuza na kuheshimu mipango ya uwajibikaji wa wadau ambayo kwayo washirika wazawa wanaweza kutoa maoni muhimu kuhusu kinachofanyika

5 Rose, Marin na Wadham-Smith, Nick. "Mutuality, Trust, and Cultural Relations (Mapatano, Kuaminiana na Mahusiano ya Kitamaduni)" London: Counterpoint, British Council (Mkazo, Baraza la Uingereza) (2004): https://uscpublicdiplomacy.org/sites/uscpublicdiplomacy.org/files/legacy/pdfs/Mutualit-Rose.pdf

**Kuangazia Mbinu ya Mipango ya LCS: Ushirikiano wa G2G**

Msaada kutoka kwa serikali hadi serikali nyingine (G2G), ambao unarejelea mikataba ya ufadhili wa moja kwa moja kati ya USAID na serikali washirika, ni zana moja ya mipango ambayo USAID hutumia kuwezesha utendaji ulioboreshwa na matokeo ya maendeleo endelevu katika mifumo ya kizawa. Mikataba hii hutumia njia mbalimbali za ufadhili na si kamilifu yenyewe. Badala yake, hutoa njia ambayo USAID na serikali washirika wanaweza kutumia kufafanua upya mahusiano yao na kutambua "uwezo wa kushirikiana" ili kwa pamoja kushughulikia masuala muhimu zaidi ya kimataifa. Kupitia mchakato wa kuunda na kusanifu pamoja, USAID na serikali washirika hutambua malengo yaliyokubaliwa pamoja na shughuli za utekelezaji ambazo zinaweza kufanywa kupitia mifumo na taasisi za kitaifa na sehemu ndogo za kitaifa na kujitolea kuendeleza malengo haya kupitia mipango ya uwajibikaji wa pande zote. Kwa kuwa na zaidi ya mahusiano ya kawaida ya wafadhili na wafadhiliwa, ushirikiano wa G2G huwezesha umiliki wa nchi wa pamoja na kuimarisha uwezo wa sekta ya umma ili kutoa vyema zaidi na kudumisha huduma zinazokidhi mahitaji na matamanio ya wananchi wote.

MAREJELEO: [ADS Chapter 220 Strengthening the Capacity of Partner Governments through Government-to-Government (Sura ya 220 ya ADS Kuimarisha Uwezo wa Serikali Washirika kupitia Msaada kutoka kwa Serikali hadi Serikali Nyingine) (G2G)]

kwa ufanisi na kinachoweza kuboreshwa. Ili kujifunza na kuboresha, USAID lazima itafakari na kuelewa uzoefu wetu katika kuwezesha uimarishaji wa uwezo na washirika na wadau kutoka katika sekta mbalimbali, na kutoa umuhimu sawa kwa mitazamo yao kama yetu. Kushirikiana na wadau kutoka katika sekta mbalimbali kwa ajili ya ufuatiliaji, kujifunza, na kufanya marekebisho kunaweza kuwa kwa aina mbalimbali, kama vile kuunda nadharia za mabadiliko pamoja, kuchagua pamoja viashirio vya utendaji ambavyo huakisi maono ya mafanikio yanayoongozwa na wenyeji, kuchanganua na kufasiri data kwa ushirikiano, au kuweka vipaumbele vya hatua za kurekebisha mpango kwa ushirikiano. Bila kujali aina, kwa kupeleka eneo la kujifunza na kufanya marekebisho karibu na wadau wazawa, USAID inaweza kuwezesha uongozi na umiliki wa kizawa.



# IV. KUFANYA MABADILIKO KUWA KAIDA YA TAASISI: MWELEKEO WA KUSONGA MBELE

> "Shirika litaendelea kufanya Uimarishaji Uwezo wa Wazawa kuwa jambo la msingi katika jinsi tunavyofikiri kuhusu kufikia, kupima na kudumisha matokeo ya kibinadamu na maendeleo."

Sehemu za awali za sera hii zinaeleza maono kuhusu kwanini na jinsi ya kuwekeza katika uwezo wa wadau kutoka katika sekta mbalimbali kulingana na uelewa wa pamoja wa kanuni za uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa. Ili kupata matokeo kamili yanayoweza kutokana na maono haya, sera, desturi na michakato ya Shirika lazima ifungamanishe kanuni zilizoelezwa hapo awali. Kutokana na hilo, sehemu hii inaangazia mbinu ya udhibiti wa mabadiliko ambayo kwayo Shirika litaendelea kufanya Uimarishaji Uwezo wa Wazawa kuwa jambo la msingi katika jinsi tunavyofikiri kuhusu kufikia, kupima na kudumisha matokeo ya kibinadamu na maendeleo. Mbinu hizi pia ni muhimu kwa washirika wa kimataifa na wafadhili wengine, ukizingatia jukumu muhimu wanalotekeleza katika kuwezesha Uimarishaji Uwezo wa Wazawa.

Mchakato wetu wa jumla wa udhibiti wa mabadiliko lazima uanze kwa kutambua mazingira, mitazamo, miundo na desturi za utendaji ambazo zinaweza kuwa vikwazo katika kufikia matamanio ya sera. Kwa mfano, wafanyakazi wa sasa wa USAID hawatoshi na wafanyakazi hawana motisha ya kuwezesha ushirikishaji wa kina na wa muda mrefu zaidi na washirika wa ndani. Kwa hivyo, maono ya sera hii yanahitaji mabadiliko ya kimuundo na motisha za kimkakati ili kuwatia motisha na kuwawezesha wafanyakazi kufanya kazi kwa njia mpya. Kushughulikia masuala haya kwa ufanisi pia kunahitaji uwajibikaji wa kitaasisi uliofafanuliwa hapa chini.

Tathmini za sera za hivi karibuni zinaonesha usaidizi endelevu, thabiti na ulioratibiwa wa ngazi ya uongozi kuwa kichocheo kikuu kwa ufanisi wa utekelezaji wa sera[6]. Kwa sera hii, uongozi huu utachukuliwa na vitengo vinavyohudumu katika ngazi tatu.

Katika ngazi ya juu zaidi, Baraza jipya lililobuniwa la Ushauri wa Sera (PAC), linalojumuisha viongozi waandamizi wa Shirika, litatoa uratibu wa ngazi ya juu na kutoa ushawishi kwa ahadi zinazohitajika ili kutimiza vipaumbele vya USAID vya maendeleo na usaidizi wa kibinadamu, ikiwa ni pamoja na Kuimarisha Uwezo wa Wazawa.

Katika ngazi ya pili, kamati ndogo ya PAC, inayoongozwa na Ofisi ya Maendeleo, Demokrasia na Uvumbuzi (DDI),

6 Matokeo haya yanatokana na mfululizo wa Tathmini za Utekelezaji wa Sera (PIA) zilizofanywa na USAID.

USAID. "Policy Implementation Assessment of the Local systems Framework (Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Utaratibu wa Mifumo ya Ndani)" (Januari 2021): https://pdf.usaid.gov/pdf_docs/PA00Z8CG.pdf.

USAID. "Policy Implementation Assessment of the USAID's Building Resilience to Recurrent Crisis (Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Mpango wa USAID wa Kukuza Ustahimilivu Dhidi ya Mgogoro wa Mara kwa Mara): Policy and Program Guidance-Executive Summary (Mwongozo wa Sera na Mpango-Muhtasari wa Utendaji)" (Novemba 2021): https://pdf.usaid.gov/pdf_docs/PA00ZDBM.pdf.

Picha kwa Hisani ya: André Josué Anchecta Oseguera

inatazamiwa kutoa uangalizi wa moja kwa moja zaidi kwa uongozi unaohusu sera hii, hivyo kuthibitisha kwamba utendaji na mipango ya Shirika inazidi kuakisi kanuni zilizowekwa katika sera na kuidhinisha hatua zilizopewa kipaumbele zinazowekwa katika mipango ya utekelezaji ya kila mwaka. Katika ngazi ya kazi, Timu ya Utekelezaji ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa (LCS) ya Shirika zima, inayoongozwa na Kitengo cha Ubia wa Kizawa, Imani na Mageuzi (DDI/LFT) kwa ushirikiano wa karibu na Ofisi ya Usimamizi (M) na Ofisi ya Sera, Mipango na Kujifunza (PPL), itawajibika kubuni mipango ya kila mwaka na kuratibu utekelezaji wake. Mipango hii ya utekelezaji itashughulikia maeneo manne yanayopishana ambayo yamepewa kipaumbele.

## 1. Fanya Uwajibikaji Kuwa Kaida ya Taasisi katika Uongozi wa USAID ili Kuendeleza Mageuzi

Ndani ya mwongo mmoja uliopita, USAID imepata maendeleo makubwa—kuanzia Mageuzi ya Utekelezaji na Ununuzi (IPR), hadi Masuluhisho ya Kizawa hadi Ubia Wenye Ufanisi na Mageuzi ya Ununuzi (EPPR), hadi kujitolea upya kwa ujanibishaji na kukuza kanuni za utofauti, usawa,



Picha kwa Hisani ya: USAID/Sayora Khalimova

ujumuishaji na ufikikaji (DEIA)—kuhusiana na kuboresha mwongozo wa mipango na desturi za ununuzi na usaidizi ili kuwezesha Kuimarisha Uwezo wa Wazawa. Ingawa kanuni zilizoelezwa katika sera hii zinajikita katika kazi iliyokamilishwa chini ya juhudi hizo, Shirika litahitaji kuendelea kutambua na kushughulikia vizuizi na vikwazo ili kufungamanisha kanuni za Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kwa ufanisi katika michakato yote ya USAID ya mipango na ununuzi na usaidizi. Ili kufanikiwa, viongozi wa Shirika lazima wawapatie wafanyakazi motisha, rasilimali na uwezo wa kufanya marekebisho yanayohitajika ili kutekeleza Kuimarisha Uwezo wa Wazawa. Kutokana na hilo, mipango ya utekelezaji ya kila mwaka ya LCS itatambua fursa mahususi ambapo viongozi wa Shirika wanaweza:

- Kuratibu na Ofisi ya Usimamizi, Ofisi ya Udhibiti wa Bajeti na Rasilimali (BRM), Ofisi ya Udhibiti wa Rasilimali Watu na Talanta (HCTM), na Ofisi nyingine husika na Ofisi Huria (B/IOs) ili kupata rasilimali zinazohitajika kubuni mazingira mazuri ya uendeshaji, kupata wafanyakazi na kuwatia motisha, na kupata ufadhili wa mipango inayofungamana na LCS.

- Kushirikisha kamati husika za bunge kuunga mkono utoaji wa rasilimali za kutosha kufadhili na kuwezesha usimamizi wa mipango ya LCS.

- Kutoa habari kuhusu kujitolea kuliko endelevu kwa USAID kwa kanuni zilizoelezwa katika sera hii.

## 2. Tanguliza Uwajibikaji wa USAID kwa Wadau wa LCS

Timu ya Utekelezaji ya LCS itaratibu juhudi pana ya kutanguliza uwajibikaji kwa wahusika na wadau wazawa ili kupata rasilimali za kutosha zilizotengwa kwa ajili ya kufanya majaribio, uvumbuzi na utendaji unaofaa zaidi katika Kuimarisha Uwezo wa Wazawa. Juhudi hii itajumuisha:

- Kuinua, kufadhili na kusambaza desturi za utendaji zinazotokana na ushahidi na zinazofaa zaidi kwa ufuatiliaji, tathmini na mbinu za kujifunza katika mipango ya kuimarisha uwezo.

- Kufadhili mitandao wenza, jamii za utendaji, na/au vituo vya rasilimali ambavyo vimetengwa kwa vitendo vya uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa.

- Kupanua mazungumzo na wadau kutoka katika sekta mbalimbali kwa kuomba maoni ya kila mwaka na kufanya vikao vya kusikiliza na kuwashirikisha katika tathmini za sera.

- Kukuza utamaduni unaozingatia mapatano ambao hutunza mahusiano ya kuaminiana na washirika wazawa, kuheshimu uwezo wao uliopo na kufuata vipaumbele vyao vya kuimarisha uwezo.

Ili kutoa uwajibikaji, Timu ya Utekelezaji itafanya tathmini ya utekelezaji wa sera miaka mitano baada ya kuchapishwa kwa sera ili kutathmini ufanisi wa mipango yetu ya LCS. Maoni kutoka kwa wadau kutoka katika sekta mbalimbali yatakuwa sehemu muhimu ya tathmini hii.

## 3. Jumuisha Utendaji wenye Ufanisi wa Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kwenye Mwongozo na Rasilimali za Mzunguko wa Mpango wa USAID.

Mzunguko wa Mpango ni muundo wa uendeshaji wa USAID wa kupanga, kutoa, kutathmini na kurekebisha mipango ya maendeleo ulimwenguni kote. Mwendelezo wa kipaumbele cha Timu ya Utekelezaji ya LCS kitakuwa kushirikiana kwa karibu na PPL na Ofisi ya Ununuzi na Usaidizi ya Ofisi ya Usimamizi (M/OAA) ili kufanya kuwa kaida za taasisi kanuni na desturi za uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa zilizoelezwa katika sera hii katika vipengele vyote vya Mzunguko wa Mpango, ikiwa ni pamoja na kupitia mwongozo, zana, mafunzo na rasilimali nyingine mpya zinazowawezesha wafanyakazi walio kwenye nyanja za kuendeleza utendaji huu.

Kipaumbele cha awali kitakuwa kusasisha mwongozo mkuu wa Mzunguko wa Mpango wa USAID ili kuakisi na kuendeleza kanuni zilizobainishwa katika sera hii. Timu ya Utekelezaji ya LCS itashirikiana na wafanyakazi wenzao wa PPL kutambua mahali ambapo mwongozo wa sasa unaweza kurekebishwa au kuzidishwa ili kulingana katika mpangilio mzima wa michakato ya Mzunguko wa Mpango—kuanzia mkakati, mradi na muundo wa shughuli; hadi ufuatiliaji, tathmini na kujifunza; hadi fedha zinazotolewa na serikali moja kwa serikali nyingine.

Wakati huo huo, na kwa kutambua kwamba Kuimarisha Uwezo wa Wazawa kunahitaji kurekebishwa ili kufaa kwa mazingira maalum, Timu ya Utekelezaji ya LCS itashirikiana na Ofisi za utendaji kazi za USAID kubuni mwongozo wa utekelezaji unaojumuisha kanuni za LCS katika mipango ambayo hushughulikia masuala mahususi ya kisekta au uendeshaji. Miongozo hii itakuwa kipaumbele katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa sera na itahitaji kuidhinishwa na kamati ya PAC inayoangazia Kuimarisha Uwezo wa Wazawa.

Kando na mwongozo wa mipango, Timu ya Utekelezaji ya LCS itatambua desturi nyingine za Shirika ambazo hukwamisha uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa, hasa wakati masuala hayo yanapochukua nafasi ya malengo ya mipango. Muhimu zaidi itakuwa kushirikiana na M/OAA ili kutambua na kuondoa vizuizi vya udhibiti ambavyo huzuia kukubaliwa kwa kanuni na desturi zilizobainishwa katika sera hii.

## 4. Buni Zana na Rasilimali za Kuwatia Motisha na Kuwasaidia Wafanyakazi

Ubunifu na utoaji wa mafunzo, zana, motisha kwa wafanyakazi na bidhaa mpya za mawasiliano ni muhimu kwa wafanyakazi wa USAID, washirika na wadau wengine kuwa na ujuzi na zana zinazohitajika ili kutekeleza sera kwa ufanisi. Mageuzi na rasilimali hizi zitawawezesha wataalamu wa maendeleo kufanya mabadiliko ya mienendo yanayohitajika ili kutekeleza Kuimarisha Uwezo wa Wazawa. Miongoni mwa yaliyo muhimu zaidi ni:

- Kubuni na kutekeleza mkakati wa ndani na nje wa ushirikishaji ili kukuza sera, kuelimisha wahusika wakuu itamaanisha nini kwenye kazi yao, na kushirikiana moja kwa moja na wadau kutoka katika sekta mbalimbali na washirika wa kimataifa kutoa mkakati huo.

- Kuanzisha, kudumisha, kuratibu na kukuza Kituo thabiti cha Rasilimali cha uimarishaji wenye ufanisi wa uwezo wa wazawa kwenye ProgramNet.

- Kuhakikisha kwamba mafunzo ya Shirika, ikiwa ni pamoja na matoleo ya msingi kutoka kwa PPL na M/OAA yanajumuisha kanuni na desturi za utendaji wa sera.

- Kupendekeza mabadiliko katika Uwezo wa Msingi na Matriki ya Ujuzi wa Huduma ya Kigeni inayohusika ili kujumuisha motisha za wafanyakazi za Shirika na michakato ya kuajiri na kupandishwa vyeo na sera.

- Kuwawezesha zaidi wafanyakazi wa Kitaifa wa Huduma ya Kigeni (FSN) wa Shirika kama rasilimali muhimu kwa ushirikishaji, ubia na Kuimarisha Uwezo wa Wazawa.

Timu ya Utekelezaji ya LCS itakuwa na jukumu la kutambua hatua maalum, kupitia mpango wa utekelezaji wa kila mwaka ili kuendeleza ajenda hii.

Hata hivyo, kufanya mipango hiyo kuwa mageuzi halisi—na kanuni za LCS kuwa matendo halisi—kutahitaji kujitolea, ubunifu na ujasiri kutoka kwa ofisi nzima ya USAID. Ili kufanikiwa, mwongozo dhahiri, uvumbuzi unaoweza kutekelezeka na michakato iliyopangwa lazima ioanishwe na uongozi thabiti, rasilimali za kutosha na mabadiliko katika uelewa wa ushirikiano wa maendeleo. Ni kwa mabadiliko haya ya kimfumo tu ndani ya USAID tutaweza kutimiza maono yetu ya pamoja ya Kuimarisha Uwezo wa Wazawa.



Picha kwa Hisani ya: Feed the Children/Amos Gumulira

USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI

**U.S. Agency for International Development**
1300 Pennsylvania Avenue, NW
Washington, DC 20523
Simu: (202) 712-0000
Faksi: (202) 216-3524
www.usaid.gov